



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MAAMUZI YA BARAZA JUU YA TUHUMA ZA UKIUKWAJI WA MAADILI YA  
KITAALUMA KWA WAUGUZI NA WAKUNGA NCHIN**

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni mamlaka ya kisheria, iliyoundwa kusimamia taaluma na wanataaluma ya Uuguzi na Ukunga Tanzania. Baraza linafanya kazi chini ya sheria, ya **“The Nursing and Midwifery Act., 2010.**


Baraza la Uuguzi Na Ukunga Tanzania lilifanya kikao chake cha 214, tarehe 25 – 27 Januari, 2024. Katika kikao hicho, Baraza lilijadili mambo mbalimbali ya kiutendaji, ikiwa ni pamoja na kusikiliza kwa kina tuhuma mbalimbali za ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga, zilizokuwa zikiwakabili wauguzi na wakunga Watatu. Tuhuma hizo zilisikilizwa kikamilifu; na kutolewa maamuzi kama ifuatavyo;

- 1. John Chuma Baisi**, Afisa Muuguzi msaidizi (RN) kutoka katika Zahanati ya Buheloi, **Lushoto Tanga**. Muuguzi huyu aliacha kumhudumia mzazi ipasavyo aliyehitaji huduma za uzazi kinyume na Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ya Mwaka 2010. Pia alishindwa kukidhi viwango vya taaluma na kuacha kutoa huduma kwa kuzingatia weledi na maadili ya taaluma. Vilevile, alichukua fedha za mteja ndani ya Zahanati ya Serikali kinyume na sheria. Baraza limempa adhabu ya **Kumuondoa kwenye rejesta ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**. Hivyo, muuguzi **John Chuma Baisi** haruhusiwi tena kufanya kazi ya Uuguzi na ukunga.
- 2. Michelina Gwido Mduda**, Muuguzi mkunga ngazi ya cheti (EN) kutoka Zahanati ya Mtimbwa Sumbawanga. Muuguzi huyu alishindwa kumhudumia mama mzazi baada ya kujifungua, aliyehitaji huduma yake kinyume na Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ya Mwaka 2010. Pia alishindwa kusimamia viwango vya taaluma na kutoa huduma kwa kuzingatia weledi na maadili ya taaluma Baraza limempa adhabu ya **Karipio Kali**.

**Leticia Kokutebesa Muganyizi**, Muuguzi mkunga ngazi ya cheti (EN) kutoka zahanati ya Kashai, Manispaa ya Bukoba. Muuguzi huyu alishindwa kusimamia viwango vya taaluma na kutoa huduma kwa kuzingatia weledi na maadili ya taaluma ,kinyume na Sheria ya Uuguzi na ukunga Tanzania ya Mwaka 2010. Aidha, muuguzi huyu alishindwa kuwahudumia akina mama wawili waliofika kupata huduma ya kujifungua katika Zahanati ya Kashai. Baraza limempa adhabu ya **Kumuondoa kwenye Orodha ya Uuguzi na Ukunga**. Muuguzi **Leticia Kokutebesa Muganyizi** haruhusiwi tena kufanya kazi ya Uuguzi na Ukunga.

Adhabu hizi zimeainiswa katika sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 vifungu vya 25(3) (f), (g) na (k) na 28(3) (a) na (c) vya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ya Mwaka 2010.

Baraza linawakumbusha Wauguzi na Wakunga wote popote walipo, kuhakikisha wanatoa huduma kwa weledi na kufuata Taratibu, Kanuni na Sheria. Baraza litaendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watakaokwenda kinyume na Maadili ya taaluma hii ili kuzuia vifo visivyo vya lazima.



Prof. Lilian Mselle  
**Mwenyekiti,**  
**Baraza la Uuguzi Na Ukunga Tanzania**  
**28.01.2023**